

SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA



MAFUNZO PAMOJA NA USAJILI WA MAJENGO NA BIDHAA ZA CHAKULA NA VIPODOZI KWA WAFANYABIASHARA WA MKOA WA TANGA

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) linapenda kuwafahamisha wafanyabiashara, wenye mahoteli, mighahawa, maduka, maghala, stoo, waagizaji na wadau wengine wa bidhaa za chakula na vipodozi hapa nchini kuwa, tarehe **24 Septemba, 2020** kuanzia **saa 0230 asubuhi** hadi **saa 1000 jioni** kutakuwa na mafunzo ambayo yataenda sambamba na zoezi la usajili wa majengo na bidhaa za chakula na vipodozi. Mafunzo haya pamoja na usajili huu utafanyika katika **ukumbi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga**.

Mafunzo na usajili umelenga kutoa elimu kuhusu usajili, madhara ya vipodozi vyenye viambata sumu pamoja na kufanya usajili kwa walengwa ikiwa ni pamoja na wale ambao hawajafanya usajili wa maeneo yao au vyeti vya usajili vilishaisha muda wa matumizi.

Kwa taarifa hii mnaombwa wadau wote kuhudhuria bila kukosa mkiwa na nakala ya leseni ya biashara (business licence) pamoja cheti cha utambulisho wa mlipa kodi (TIN Certificate). **Kwa ufafanuzi zaidi wasiliana na Bi. Janeth Kakulu simu Na. 0659 248 925**

Kwa taarifa zaidi wasiliana na:

Mkurugenzi Mkuu,

Shirika la Viwango Tanzania,

S L P 9524, Dar es Salaam.

Simu: +255 (022) 2450298; Hotline: +0800 110 827

Barua pepe: info@tbs.go.tz;

Tovuti: www.tbs.go.tz

